

**OFISI YA MKUU WA MKOA
RUMA**

Simu, 2602256/2602238

Fax Na. 2602144

Anwani ya Posta: S.L.P 74, Songea

Email; ras.ruvuma@tamisemi.go.tz/

aepe@ruvuma.go.tz

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na

Afisa Biashara wa Halmashauri

iliyeko karibu na wewe

Au wataalam Ofisi ya Biashara Mkoa

kwa simu Na.

+255763508173,+255755192064

OFISI YA MKUU WA MKOA RUVUMA

RUVUMA ITAVUMA KWA UCHUMI WA VIWANDA 'WEKEZA SASA'



**KITAMBULISHO CHA
MJASIRIAMALI MDOGO**



KITAMBULISHO CHA MJASIRIAMALI MDOGO

UTANGULIZI

Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Pombe Joseph Magufuli alikabidhi Vitambulisho vya wajasiriamali wadogo kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa siku ya tarehe 10/12/2018 ili kuvigawa kwa wajasiriamali wadogo wenye mauzo ghafi yasiyozidi Shilingi Milioni Nne kwa mwaka kwa lengo la kuwasaidia kuweza kujikwamua katika Sekta ya Biashara



Picha ya Kitambulisho cha Mjasiriamali Mdogo

FAIDA YA KUWA NA KITAMBULISHO CHA MJASIRIAMALI MDOGO

1. Kufanya biashara mahali popote ndani ya mipaka ya nchi ya Tanzania .
2. Ada ya kitambulisho hicho ni nafuu.
3. Serikali kukutambua kuwa ni mjasiriamali mdogo .
4. Kutokubughudiwa na Mamlaka yoyote kwa kuombwa ushuru .
5. Kuchangia kipato cha nchi kwa kulipa ada ya kitambulisho kwa mwaka.



Picha ya wajasiriamali wadogo wakiwa wanafanya Biashara

VIGEZO VYA KUPATA KITAMBULISHO CHA MJASIRIAMALI MDOGO

Muombaji wa kitambulisho cha Mjasiriamali mdogo anatakiwa azingatie mambo yafuatayo;

1. Awe na mauzo ghafi yasiyozidi shilingi Milioni Nne (4,000,000/=) kwa mwaka.
2. Awe hajawahi kusajiliwa na TRA na kupewa namba ya utambulisho wa Mlipa kodi (TIN).
3. Anatakiwa ajaze fomu maalum inayopatikana katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya .

MAHALI KITAMBULISHO KIN-AOPATIKANA

Vitambulisho vinapatikana katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya .

GHARAMA YA KITAMBULISHO

Kitambulisho kinatolewa kwa kulipa ada ya shilingi 20,000 kwa mwaka